# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

## KIKAO CHA HAMSINI NA SITA

**28 JUNI, 2024**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### KIKAO CHA HAMSINI NA SITA – TAREHE 28 JUNI, 2024

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**716. MHESHIMIWA JANETH ELIAS MAHAWANGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutengeneza fursa za ajira kwa Vijana kwa mfumo wa pamoja kati ya Serikali na Wadau wengine.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**717. MHESHIMIWA JACKSON GEDION KISWAGA (KALENGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kubakiza asilimia 40 ya Fedha zinazokusanywa kwenye Halmashauri kwani hali ya Kifedha kwa Halmashauri sio nzuri.

**718. MHESHIMIWA DEO KASENYENDA SANGA (MAKAMBAKO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaigawa Kata ya Kivavi - Makambako.

**719. MHESHIMIWA BONIPHACE NYANGINDU BUTONDO (KISHAPU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka Fedha Jimbo la Kishapu kupitia Mfuko wa TARURA kwa ajili ya Barabara zenye urefu wa Km 522 ambazo zimeharibika.

**720. MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifanyia ukarabati Shule Kongwe za Msingi katika Mkoa wa Dar es Salaam ambazo zipo katika hali mbaya.

## WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

**721. MHESHIMIWA DKT. ANGELINE SYLVESTER LUBALA MABULA (ILEMELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itaweka miundombinu rafiki ya kukaushia Samaki na Dagaa kwenye mialo ya Ziwa Victoria – Mwanza.

**722. MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, Serikali haioni haja ya kupanga bei elekezi kwa kilo ya Nyama na mazao mengine ya Mifugo kama ilivyo kwa mazao ya Kilimo.

## WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

**723. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, lini Muswada wa Sheria utakaokidhi Haki nane za Kimataifa za kumlinda Mtumiaji/Mlaji zilizopitishwa na Umoja wa Mataifa utaletwa.

## WIZARA YA UCHUKUZI:

**724. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Mamlaka ya Viwanja vya Ndege itaruhusiwa kukusanya na kutumia *Passenger Service Charge* kuboresha Viwanja vya Ndege.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**725. MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA (SIKONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itazalisha mbegu za Mti wa Mninga ili kuufanya Mti huo kuwa Zao la Biashara.

**WIZARA YA KILIMO:**

**726. MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani kupitia SIDO kutoa Mashine ndogo na rahisi kwa Vikundi vya Wanawake vya ubanguaji Korosho Mkoani Mtwara.

**727. MHESHIMIWA GEORGE RANWELL MWENISONGOLE (MBOZI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itawachukulia hatua Viongozi wa Vyama vya Msingi waliodhulumu fedha za Wakulima wa Kahawa - Mbozi.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**728. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali ina mkakati gani kumaliza tatizo la Vitambulisho vya NIDA kwa kuwapatia namba za NIDA Wananchi wa Wilaya ya Karagwe na Kyerwa.

**729. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itaboresha maslahi ya Askari wa Idara ya Uhamiaji.

**WIZARA YA FEDHA:**

**730. MHESHIMIWA TOUFIQ SALIM TURKY (MPENDAE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kunakuwa na muunganiko wa kodi ili kupunguza utitiri wa kodi usio wa lazima kwa Wawekezaji.

**III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:**

***(Kusomwa Mara ya Kwanza)***

(a) Muswada wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania wa Mwaka 2024.

(b) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.2) wa Mwaka 2024 *(The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.2) Bill, 2024).*

(c) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria zinazohusu Ulinzi wa Watoto *(The Child Protection Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2024).*

(d) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa *(The Prevention and Combating of Corruption (Amendments) Bill, 2024).*

## IV. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2024 *(The Finance Bill, 2024).*

***(Majadiliano yanaendelea)***

## V. TAARIFA YA KATIBU WA BUNGE:

**VI. HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE:**

**WAZIRI MKUU:**

**VII. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA AFRIKA MASHARIKI.**

**DODOMA**
**28 JUNI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc***
**KATIBU WA BUNGE**